# JARIDA LA RS RUVUMA

## MEI 2025



# MBIO ZA MWENGE WA UHURU MKOANI RUVUMA

www.ruvuma.go.tz

RS RUVUMA RS RUVUMA RS RUVUMA

## KARIBU MKOA WA RUVUMA



Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, kutoa nakala kivuli au kutoa baadhi ya maandishi ya Jarida hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Mwandishi kwa maandishi.

## JARIDA LA RS RUVUMA TOLEO MAALUM LA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MEI 2025

Jarida limehaririwa na **Albano Midelo** wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma



Kulia ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Bi. Mary Makondo akimkabidhi Mwenge wa Uhuru Mkuu wa Wilaya ya Songea Mheshimiwa Kapenjama Ndile kwenye viwanja vya shule ya msingi Igawisenga Madaba

## TAHARIRI

Wapendwa wasomaji wetu ninayoheshima kubwa kuwaalika katika Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kusoma habari na makala mbalimbali ambazo zinakuwa zinachapishwa na jarida hili.

Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia kitengo cha Mawasiliano Serikali kuhakikisha kila mwezi GCU Mkoa na Halmashauri zake zinachapisha jarida ili kutangaza shughuli mbalimbali zinazofanywa na serikali ikiwemo kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, mahusiano na kutangaza fursa za utalii na uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma na namna viongozi wa ngazi ya Wilaya,Mkoa na kitaifa wanavyofanya ziara za kuzungumza na wananchi,kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Furahia kusoma

## RC RUVUMA ALIVYOZUNGUMZA NA WANAHABARI KUHUSU MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2025



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, alisema kuwa mbio za mwenge mkoani Ruvuma zitaanza tarehe 9 Mei, 2025 ambapo mwenge huo utapokelewa katika Kijiji cha Igawisenga, Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, ukitokea Mkoani Njombe.

Akizungumza na waandishi wa habari Ofisini kwake, Kanali Ahmed alisema ni muhimu kwa wananchi wa mkoa wa Ruvuma kufahamu kuwa mwenge huo utakimbizwa katika halmashauri zote nane za mkoa wa Ruvuma.

Aliitaja ratiba ya mbio hizo katika mkoa wa Ruvuma ambapo Mei 9, 2025 ni Madaba DC, Mei 10, 2025 Songea DC, Mei 11, 2025 Mbinga DC, Mei 12, 2025 Nyasa DC, Mei 13, 2025 Mbinga TC, Mei 14, 2025 Songea MC, Mei 15, 2025 Namtumbo DC, Mei 16, 2025 Tunduru DC na tarehe 17 Mei 2025 mwenge huo utakabidhiwa mkoa wa Mtwara.

Mbio hizo kwa mwaka huu zinaongozwa na kauli mbiu inayohusu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ambayo inasema "Jitokeze Kushiriki Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kwa Amani na Utulivu," kauli mbiu hiyo inaambatana na ujumbe wa kudumu wa mapambano dhidi ya Malaria unaosema "Zero Malaria inaanza na mimi, wewe na sisi wote."

Kauli mbiu zingine ni "Kataa dawa za kulevya, timiza malengo yako," "Kuzuia rushwa ni jukumu langu na lako, tutimize wajibu wetu," na ujumbe unaohusu lishe unaosema "Afya ni mtaji wako, zingatia unachokula."



# MWENGE WA UHURU KUPITIA MIRADI 76 RUVUMA



Jumla ya miradi 76 yenye thamani ya Zaidi ya shilingi bilioni 95 inatarajiwa kutembelewa na Mwenge wa Uhuru mwaka 2025 katika Mkoa wa Ruvuma.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed wakati anazungumza na wanahabari ofisini kwake mjini Songea kuhusu mbio maalum za Mwenge wa Uhuru ambao unaanza mbio zake mkoani Ruvuma Mei 9 na kukamilisha Mei16 mwaka huu.

Amesema miradi hiyo inajumuisha sekta muhimu kama afya, elimu, maji, barabara na huduma nyingine za kijamii na kwamba Kati ya miradi hiyo,miradi 17 itazinduliwa rasmi,miradi13 itawekewa jiwe la msingi na 33 itakaguliwa ili kuona utekelezaji wake.

Ameongeza kuwa miradi mingine 13 itahusisha ugawaji wa vifaa mbalimbali kwa wananchi. Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma na kwamba miradi hiyo inaonesha dhamira ya Serikali kuleta maendeleo ya kweli kwa wananchi.

Kwa mujibu wa ratiba ya mbio hizo, Mwenge wa Uhuru utakimbizwa kuanzia Mei 9 hadi 16, 2025 katika Halmashauri zote nane za Mkoa wa Ruvuma kwa umbali wa jumla ya kilomita 1,378.90.

“Mwenge huo utaanza Halmashauri ya Madaba, kupita Songea, Mbinga, Nyasa, Mji wa Mbinga, Manispaa ya Songea, Namtumbo na kumalizia Tunduru’’,alisema Kanali Abbas.

Katika hotuba yake kwa wanahabari, Kanali Ahmed ameutaja ujumbe mkuu wa Mwenge wa Uhuru 2025 kuwa ni *“Jitokeze kushiriki Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kwa amani na utulivu”*, ambao unalenga kuhamasisha wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujitokeza kwa wingi katika uchaguzi mkuu ujao.

Mbali na kauli mbiu kuu hiyo,mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka huu pia zimejikita katika kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa lishe bora, mapambano dhidi ya rushwa, VVU/UKIMWIna matumizi ya dawa za kulevya na malaria.

Kanali Ahmed amebainisha kuwa kampeni hizi zinaendelea kuwa silaha muhimu za kujenga taifa lenye afya, maadili na ustawi wa jamii.

Ametoa rai kwa wananchi wa Ruvuma kujitokeza kwa wingi kushiriki katika mapokezi ya Mwenge wa Uhuru na kushuhudia hatua za utekelezaji wa miradi yao.

Amesisitiza kuwa Mwenge wa Uhuru si tu ishara ya historia ya uhuru, bali pia chombo cha kuangaza maendeleo, ushirikiano na maandalizi ya uchaguzi wa amani mwaka 2025.



Baadhi ya wananchi waliojitokeza kumsikiliza kiongozi wa mbio za mwenge wa uhuru kitaifa 2025 Ndugu İsmail Ali Ussi katika viwanja vya mji mdogo Lusewa wilayani Namtumbo

## MWENGE WA UHURU WAIKUBALI MIRADI YOTE MADABA




Mbio za Mwenge wa Uhuru zimeanza rasmi leo Mei 9, 2025, mkoani Ruvuma kwa kutembelea, kukagua na kuweka mawe ya msingi katika miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba.

Mwenge wa Uhuru umezindua vyumba viwili vya madarasa ya awali na matundu sita ya vyoo katika Shule ya Msingi Mkwera, umeweka mawe ya msingi katika ujenzi wa nyumba ya wageni katika Kijiji cha Lituta na mradi wa maji kijiji cha Gumbiro na kukagua mradi wa lishe katika Kijiji cha Lutukira.

Akiweka jiwe la msingi katika mradi wa maji katika kijiji cha Gumbiro, Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa, Bw. Ismail Ali Ussi, amehimiza mamlaka husika kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati ili wananchi wanufaike na juhudi zinazofanywa na serikali ya awamu ya sita na kuwasihi wananchi kutunza miradi hiyo.

Kwa upande wake Mbunge wa Madaba, Mhe. Joseph Mhagama, amesema jimbo hilo katika kipindi cha uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia limepokea bilioni 12.9 kwa ajili ya miradi ya maji.

Ameeleza kuwa mradi huo wa Gumbiro ni moja kati ya miradi ambayo inatarajiwa kukamilika hivi karibuni na mradi huo utakuwa na uwezo wa kubeba maji lita 75,000 na kuhudumia wakazi zaidi ya 2,000.

Mwenge wa Uhuru pia umekagua shughuli za kiuchumi zinazofanywa na vijana wa bodaboda katika Kijiji cha Mbangamawe na kuweka jiwe la msingi katika kituo cha kulelea watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu cha Hope Village na kushiriki katika upandaji wa miti ili kuhamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira.

## KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU AONYA KUHUSU RUSHWA KWENYE UCHAGUZI




Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2025, Ismail Ally Ussi, ametoa onyo kali dhidi ya vitendo vya rushwa, akisisitiza kuwa ni tishio kwa demokrasia, haki na maendeleo hasa katika kipindi hiki kuelekea Uchaguzi Mkuu wilayani Songea, mkoani Ruvuma.

Akizungumza katika viwanja vya Shule ya Msingi Igawisenga, Halmashauri ya Madaba, Ussi alitoa ujumbe mzito kwa viongozi wa Serikali, vyama vya siasa na wananchi, akiwataka kujitenga kabisa na vitendo vya rushwa vinavyoweza kuhatarisha uchaguzi huru na wa haki.

“Rushwa ni adui mkubwa wa haki na uwajibikaji. Ni lazima tupambane nayo kwa nguvu zote ili kulinda misingi ya uchaguzi wa kidemokrasia,” alisisitiza Ussi huku akihimiza mshikamano wa kitaifa katika kuikataa.

Katika ziara hiyo ya kukagua na kuzindua miradi ya maendeleo, Ussi aliwataka Watanzania kuwa walinzi wa maadili na kuhakikisha kuwa kila hatua ya mchakato wa uchaguzi inazingatia uwazi na uadilifu, bila kuruhusu ushawishi wa kifedha au upendeleo.

Ussi alihitimisha kwa kueleza kuwa Mwenge wa Uhuru si tu alama ya historia, bali pia ni mwanga wa kupambana na maovu kama rushwa, akitoa rai kwa kila mmoja kuenzi ujumbe huo kwa vitendo ili kudumisha amani, umoja na maendeleo ya kweli.



Moja ya shule za kisasa iliyowekewa jiwe la msingi na Kiongozi wa Mbio za mwenge wa Uhuru 2025 Ismail Ali Ussi Katika Kata ya Betheremu Halmashauri ya Mbinga Mji

**MWENGE WA UHURU ULIVYOKABIDHIWA HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA**



pichani ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Madaba Sajid Idrisa Mohamed akimkabidhi mwenge wa Uhuru Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea Elizabeth Gumbo Mwenge ndani ya viwanja vya shule ya msingi Peramiho Mwenge huo ulipitia miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 1.6



Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Mary Makondo ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kwenye mapokezi ya mwenge wa Uhuru kutoka Mkoa wa Njombe eneo la Igawisenga Madaba Mei 9 mwaka huu

# MWENGE WA UHURU WAZINDUA JENGO LA EMD PERAMIHO




Mwenge wa uhuru umeendelea na mbio zake mkoani Ruvuma katika halmashauri ya Wilaya ya Songea na kuzindua jengo la matibabu ya wagonjwa wa dharura (EMD) katika hospitali ya rufaa ya misheni ya Mt. Joseph Peramiho.

Akitoa taarifa ya mradi wa jengo hilo, Mhandisi wa Hospitali hiyo, Greyson Nyirenda, amesema hospitali hiyo ilipata kiasi cha fedha Bilioni 1,317,870,928.58 kutoka kwa wafadhili ambao ni shirika la kidini kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo.

Amebainisha kuwa mwaka 2022 idara hiyo ya wagonjwa wa dharula ilihudumia wagonjwa 49,263, mwaka 2023 wagonjwa 61,233 na baada ya kukamilisha ujenzi wa jengo hilo Novemba 2024 mpaka sasa wagonjwa 13,922 wameshahudumiwa.

Akizungumza katika hospitali hiyo kiongozi wa mbio za mwenge kitaifa 2025, Bw. Isamail Ali Ussi, amesema kama kiongozi wa mbio za mwenge na wenzake wana imani kubwa na hospitali hiyo katika kutoa huduma za afya kwa wananchi.

Naye Waziri wa Afya na Mbunge wa Jimbo la Peramiho, Mhe. Jenister Mhagama, amesema hospitali hiyo imekuwa ni kitovu cha huduma za afya kwa kuwa wananchi wa nyanda za kusini wanafika kupata huduma katika hospitali hiyo.

Ameeleza kuwa Serikali inaendelea kushirikiana na taasisi za kidini na sekta binafsi ili kuhakikisha huduma za afya zinazidi kuwa bora na kuimarika katika nchi akisisitiza kuwa sekta hizo si washindani bali ni washiriki wa Serikali katika kutoa huduma bora za afya kwa wananchi.




Kushoto ni kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2025 Ndugu Ismail Ali Ussi akisalimiana na Askofu wa Jimbo katoliki Mbinga Mhashamu John Ndimbo mjini Mbinga

# KIONGOZI  MWENGE WA UHURU APANDA MTI SONGEA



Pichani ni Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Bw. Ismail Ali Ussi, akipanda mti katika Shule ya Msingi Matomondo, Halmashauri ya Wilaya ya Songea, mkoani Ruvuma.

Zoezi hilo ni sehemu ya kuhamasisha uhifadhi wa mazingira, likilenga kuhamasisha jamii kupanda miti ili kulinda mazingira na kupunguza athari za ukataji wa miti hovyo.

Kupitia jitihada hizo, Mwenge wa Uhuru unasihi wananchi kushiriki kikamilifu katika utunzaji wa mazingira, kwani ni jukumu la kila mmoja kuhakikisha ardhi inabaki kuwa rafiki kwa kizazi cha sasa na kijacho.

# MWENGE WA UHURU WAWEKA JIWE LA MSINGI SHULE YA AMALI SONGEA



Mwenge wa Uhuru umeweka jiwe la msingi katika ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Amali katika kijiji cha Lundusi, Halmashauri ya Wilaya ya Songea, mkoani Ruvuma.

Mradi huo unagharimu shilingi milioni 560.5, ukiwezeshwa na wahisani kupitia Serikali Kuu chini ya mpango wa kuboresha elimu ya sekondari (SEQUIP).

Shule hiyo inalenga kuimarisha sera na mitaala ya elimu ili kuwawezesha wahitimu kupata maarifa na ujuzi wa ujasiriamali, hatua itakayowasaidia kujitegemea na kuchangia maendeleo ya taifa.

Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa, Bw. Ismail Ali Ussi, wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi amesema kuwa shule za amali zinajengwa ili wilaya na halmashauri izalishe wataalam wa sekta mbalimbali, kwa lengo la kupunguza utegemezi.

Amesisitiza kuwa Serikali, chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imewekeza fedha nyingi katika miradi mikubwa na ya kimkakati, hivyo wananchi wanapaswa kuunga mkono jitihada hizo na kulinda miundombinu inayojengwa.

Shule hiyo itawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo katika sekta mbalimbali, zikiwemo viwandani, mashambani, uvuvi, na ujuzi wa kujiajiri au kuajiriwa kulingana na mahitaji ya soko la ajira na mabadiliko ya teknolojia.



Mwenge wa Uhuru umeendelea na mbio zake katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga mkoani Ruvuma kwa kukagua mradi wa jengo la wagonjwa wa nje OPD katika zahanati ya Mtakatifu Gabriel inayomilikiwa na kanisa katoliki Jimbo katoliki la Mbinga.Mradi mzima uliogharimu zaidi ya shilingi milioni 100 umekamilika na unatoa huduma kwa wagonjwa wa nje OPD,wagonjwa wanalazwa pia inatolewa huduma ya mama na mtoto

## MWENGE WA UHURU WAIKUBALI MIRADI YOTE MBINGA




Mwenge wa Uhuru 2025 umeikubali miradi yote tisa yenye thamani ya shilingi bilioni1.6 iliyopitiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma.

Miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na mradi wa maji safi na salama katika gereza la kilimo Kitai ambao umefunguliwa na Mwenge wa Uhuru ukiwa na uwezo wa kuhudumia wakazi1468.

Akitoa taarifa ya mradi huo kwa Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru ,Meneja wa RUWASA Wilaya ya Mbinga Mashaka Sinkala alisema mradi huo umegharimu Zaidi ya shilingi milioni 400 kutoka serikali kuu.

Mradi mwingine uliozinduliwa na Mwenge wa Uhuru katika Halmashauri ya Wilaya Ya Mbinga ni mradi wa jengo la huduma ya mionzi katika hospitali ya Mtakatifu Gaudensia iliyopo Mkako.

Akitoa taarifa ya mradi huo ,Mkurugenzi wa Hospitali ya Mtakatifu Gaudensia Dr.Thadei Kinyero alisema jengo hilo linatoa huduma na ambazo alizitaja kuwa ni huduma ya mionzi,kipimo cha kutambua hali ya

moyo,radiolojia na kipimo cha umeme wa moyo na kwamba hadi sasa jengo hilo limetoa limetoa huduma ya wagonjwa 4049.

Hata hivyo amesema mradi huo wa jengo la radiolojia umegharimu Zaidi ya shilingi milioni 435.

Mradi mwingine ambao umepitiwa na mwenge wa Uhuru ni mradi wa uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji katika shule ya msingi Kiamili kijiji cha Kigonsera ambapo wanafunzi wameweza kuchimba mabwawa manne kwa gharama ya shilingi 700,000.

Mwenge wa Uhuru pi umetembelea mradi wa uwekezaji katika shamba la miti la Mbuji lenye ukubwa wa hekari 65.7 zenye thamani ya Zaidi ya shilingi milioni 29.

Mwenge wa Uhuru pia umepita katika mradi wa ,mabweni mawili katika shule ya sekondari Mbuji ambapo serikali imetoa Zaidi ya shilingi milioni 275 kutekeleza mradi huo.

Miradi mingine iliyopitiwa na Mwenge wa Uhuru ni mradi wa klabu ya wapinga rushwa na shamba la kahawa la mkulima binfasi Herbahat Raphael lililopo katika kijiji cha Nyoni.

Akizungumza kwa nyakati tofauti wakati anakagua miradi hiyo,Kiongozi wa Mwenge wa Uhuru kitaifa 2025 Ndugu Ismalil Ali Ussi amewapongeza viongozi katika ngazi zote na wananchi wilayani Mbinga kwa kusimamia utekeleza wa miradi hiyo ambayo inakwenda kuleta manufaa makubwa kwa wananchi.

Amesema Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan amekuwa anatoa fedha nyingi zikiwemo za maji,afya,barabara na elimu ili kuhakikisha wananchi wanatatuliwa changamoto mbalimbali zinazowakabili.

Ametoa rai kwa wananchi wote waliojiandikisha kuhakikisha wanajitokeza kwenye uchaguzi mkuu kupiga kura mwezi Oktoba ili kuwachagua madiwani,wabunge na Rais.

## WANANCHI MAGUU WAJITOKEZA KATIKA MWENGE WA UHURU



Baadhi ya wananchi wa kijiji cha Maguu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma wakiwa wamejitokeza kwa wingi kumsikiliza Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2025 Ndugu Ismail Ali Ussi



**MAHABA YA WANANCHI WA MBUJI KWA MWENGE WA UHURU**



Baadhi ya wananchi wa kijiji cha Mbuji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma wakiwa wamejitokeza kwa wingi kumsikiliza Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2025 ndugu Ismail Ali Ussi



## MWENGE WA UHURU WAPONGEZA MIRADI YA MBINGA MJI



Mwenge wa uhuru umeendelea na mbio zake mkoani Ruvuma kwa kupitia miradi kumi yenye thamani ya shilingi bilioni 1.2 katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga.

Kiongozi wa mbio za mwenge kitaifa wa uhuru 2025 Ndugu Ismail Ali Ussi amepongeza usimamizi wa miradi ya maendeleo uliofanywa na viongozi kwa kushirikiana na wananchi hali iliyosababisha miradi kuwa na viwango bora.

Moja ya miradi iliyopitiwa na mwenge wa uhuru ni ujenzi wa shule mpya ya sekondari Kata ya Betherehemu ambapo serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 740 kutekeleza mradi huo kupitia program ya uboreshaji elimu ya sekondari (SEQUIP).

Mwenge wa uhuru pia umekagua na kufungua mradi wa maji Mkwaya unaokadiriwa kugharimu Zaidi ya shilingi milioni 375 na unatarajia kuhudumia wananchi 1,853.

Meneja wa RUWASA wilaya ya Mbinga Mhandisi Yona Ndomba amesema hadi sasa utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 100 na tayari kaya 13 zimeunganishwa na huduma ya maji majumbani.

Mwenge wa uhuru ukiwa katika Halmashauri ya mji wa Mbinga umekagua mradi wa huduma za afya zinazotolewa na jengo la OPD katika zahanati ya Mtakatifu Gabriel inayomilikiwa na Jimbo katoliki la Mbinga.

Askofu wa Jimbo la Mbinga Mhashamu John Ndimbo amesema ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje OPD ni sehemu tu ya ujenzi wa mradi mzima wa kituo cha afya tarajiwa cha St.Gabriel Jimbo katoliki la Mbinga.

Amesema mradi wa OPD umegharimu Zaidi ya shilingi milioni 100 ukiwa ni msaada kutoka kwa wafadhili na majitoleo ya waumini.

Mwenge wa uhuru ukiwa katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga pia umekagua mradi wa shamba la miti linalomilikiwa na Ndugu Lukas Nchimbi Mkazi wa kijiji cha Utiri .

Shamba hilo lina ukubwa la hekari 10.4 likiwa na jumla ya miti ya kupanda 4,600 na kwamba mradi huo una thamani ya shilingi milioni 32.

Mwenge wa uhuru pia ukiwa mjini Mbinga umetembelea na kukagua kikundi cha UMOJA kinachofanya shughuli za ufundi seremala na kuchakata mazao ya misitu ili kuongeza kipato cha wanakikundi ambapo hadi sasa mradi umegharimu shilingi milioni 33.

Akizungumza baada ya kukamilisha kupitia miradi hiyo Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2025 Ndugu Ismail Ali Ussi ameupongeza uongozi wa Wilaya,Halmashauri na wananchi kwa usimamiaji mzuri wa miradi ukiwemo mradi mpya wa shule ya sekondari Kata ya Betherehemu ambayo itawapunguzia watoto umbali wa kwenda mbali kufuata shule ya sekondari.

Amepongeza ujenzi wa shule hiyo ambayo amesema ni bora na ina viwango vinavyolingana na thamani ya fedha

“Mimi binafsi wakati naingia katika shule hii nilikuwa najiuliza hii ni shule au hoteli,mkuu wa wilaya aliniambia hii ni shule,shule kama hii tulikuwa tumezoea kuiona katika maeneo maalum kama Dar es salaam,tuna kila sababu ya kumpongeza Rais kwa kutoa fedha za ujenzi wa shule hii’’,alisisitiza Ussi.

# MWENGE WA UHURU WAMULIKA MIRADI  YA NYASA




MWENGE wa uhuru 2025 umepitia na kuridhishwa na utekelezaji wa miradi tisa yenye thamani ya shilingi bilioni 82 katika wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma.

Mkuu wa Wilaya ya Nyasa Mheshimiwa Peres Magiri amesema kati ya miradi hiyo,Mwenge wa Uhuru umekagua miradi mitatu,umeweka jiwe la msingi mradi mmoja na kuzindua miradi mitatu na miradi miwili kugawa vyandarua

Akitoa taarifa kwa Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2025,Meneja wa RUWASA Wilaya ya Nyasa Mhandisi Masoud Samila amesema utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 40 na kwamba wananchi 4,490 watapata maji safi kupitia mradi huo.

Mwenge wa Uhuru pia umezindua mradi wa mtambo za kufua hewa tiba (Oxygen plant)  ambapo kiasi cha shilingi milioni 480 zimetumika kujenga miundombinu ya gesi na ununuzi wa mtambo wa kuchakata hewa tiba.

Mradi huu umekuwa na faida kubwa katika utoaji wa huduma za afya hospitalini ikiwemo kusogeza huduma jirani na kupunguza gharama za kununua huduma.

Mwenge wa uhuru umekagua shughuli za kikundi cha wajasiriamali vijana katika kijiji cha Ruhekei Kata ya Kilosa ambapo kikundi hicho kimefanikiwa kupata mkopo wa shilingi milioni 16.5 .

Akitoa taarifa ya kikundi hicho Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Nyasa Khalid Khalif amesema mkopo huo unatokana na fedha za asilimia kumi ya mapato ya ndani ya Halmashauri hiyo.

Mradi mwingine uliozinduliwa na Mwenge wa uhuru ni ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika shule ya sekondari Limbo ambapo serikali ilitenga shilingi milioni 72 kutekeleza mradi huo.

Kukamilika kwa mradi huo kumeboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia wanafunzi hivyo kupunguza mlundikano wa wanafunzi darasani.

Mwenge wa Uhuru pia umetembelea na kukagua mradi wa kimkakati wa ujenzi wa bandari na barabara ya kuingia bandari ya Mbambabay kwa kiwango cha zege.

Meneja wa Bandari katika ziwa Nyasa Manga Gassaya amesema serikali imetenga Zaidi ya shilingi bilioni 82 kutekeleza mradi wa bandari ya Mbambabay na kwamba mradi huo unatarajia kukamilika Januari,2026.

Mwenge wa Uhuru ukiwa wilayani Nyasa pia umepitia miradi ya wapinga rushwa katika sekondari ya Kingerekiti na utekelezaji wa shughuli za lishe ambapo wilaya hiyo imetumia Zaidi ya shilingi milioni 33 sawa na asilimia 100 kugharamia afua za lishe kwa watoto 32,574.

Mwenge wa uhuru umekagua mradi wa kugawa vyandarua vyenye thamani ya shilingi 500,000 ambapo katika wilaya ya Nyasa mwaka 2024 jumla ya watu 14,412 waliugua ugonjwa wa malaria.

Wilaya ya Nyasa inaendelea na mapambano dhini ya malaria kwa kugawa vyandarua kwa watoto chini ya miaka mitano jumla ya wajawazito 7,325 na watoto 9,114 walipatiwa vyandarua mwaka 2024.

Akizungumza baada ya kukagua miradi hiyo ukiwemo mradi mkubwa wa kimkakati  wa ujenzi bandari ya Mbambabay,Kiongozi wa mbio za Mwenge wa uhuru 2025, Ismail Ali Ussi  Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan ametoa mabilioni ya fedha kuhakikisha mradi wa bandari ya kisasa unakamilika.

“Leo hii tumekuja kujionea bandari ya kisasa inayokwenda kutuunganisha na nchi jirani.serikali imefanya uwekezaji mkubwa wa bandari,mradi ambao unatarajia kukamilika mapema mwaka 2026”,alisema.

Katika hatua nyingine Kiongozi huyo wa mwenge wa Uhuru amewakumbusha wananchi kujitokeza kwa wingi kwenye uchaguzi Mkuu Oktoba mwaka huu kwenda kupiga kura.

## NIMEUONA KWA MACHO KWA MARA YA KWANZA MWENGE WA UHURU ,NINA MIAKA 89



Kwa miaka 89 ya maisha yake, Mzee Mohamed Saidi wa Kata ya Matogoro, Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma ameshuhudia

mengi:Lakini jambo moja muhimu la kihistoria lilikuwa halijawahi kutia mguu kwenye macho yake—Mwenge wa Uhuru.

“Nimekuwa nikiusikia tu kwenye redio,kuuona kwenye picha na kuwaona wengine wakisherehekea, lakini sikuwahi kuushuhudia kwa macho yangu,” anasema kwa sauti ya upole lakini yenye msisimko, akiwa amevaa kofia yake ya zamani aliyoinunua mwaka 1972

. “Leo, hatimaye, nimeuona hapa kwangu. Sikuamini kama nitaishi hadi kuuona.”

Ni Mei14  2025. Mwenge wa Uhuru umefika Manispaa ya Songea, na moja ya sehemu zilizoguswa kwa hisia kubwa ni Bonde la Timamu, ambapo kiongozi wa mbio hizo kitaifa  Ndugu Ismail Ali Ussi amezindua mradi wa kisima cha maji asilia kilichoboreshwa—kisima ambacho kina historia ndefu kama ya Mzee Mohamed mwenyewe.

Kisima hicho, kilichojulikana na wakazi kama “chemchem ya maisha”, kimekuwa chanzo kikuu cha maji kwa wakazi wa Matogoro tangu mwaka 1950.

Kwa sasa, kutokana na juhudi za Serikali katika Manispaa ya Songea kwa usimamizi wa Mkurugenzi Wakili Bashir Muhoja, kisima hicho kimeboreshwa kwa gharama ya shilingi milioni 23.9 na kunufaisha zaidi ya kaya 500.

“Maji haya sasa ni salama zaidi, yanapatikana kwa urahisi na yanaheshimu hadhi ya mwananchi,” anasema Mkurugenzi Muhoja. “Hiki ni chanzo asilia lakini sasa kimewekewa miundombinu ya kisasa ili kuhakikisha wananchi wa Matogoro hawanyimiwi huduma ya msingi ya maji.”

Lakini jambo kubwa zaidi si tu maji, bali moyo wa ukarimu na uzalendo wa Mzee Mohamed. Eneo la kisima hicho, lenye thamani kubwa kwa sasa, alilikabidhi kwa Serikali bila kudai fidia yoyote.

“Nilifikiri, kama nisipotoa hiki kwa ajili ya jamii, nini kingine cha maana nitakachowacha?” anauliza kwa unyenyekevu. “Nimeishi hapa maisha yangu yote. Maji haya yamenilea, nimeoga hapa, watoto wangu wamecheza hapa. Sasa ni zamu ya kizazi kijacho kufaidika.”

Ujio wa Mwenge wa Uhuru haukuwa tu tukio la kitaifa, bali hadithi ya maisha ya mtu mmoja aliyesubiri kwa miongo sita kuuona. Na zaidi ya hapo, ni hadithi ya kuunganishwa kwa historia ya mtu binafsi na historia ya taifa, kupitia kisima kimoja—kisima cha Timamu.

## MWENGE WA UHURU WATINGISHA MANISPAA YA SONGEA



Mwenge wa Uhuru umeendelea kung'ara katika Mkoa wa Ruvuma baada ya kuingia rasmi katika Manispaa ya Songea Mei 14, ambapo umepitia miradi nane ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 1.8, huku ukionesha kasi na dhamira ya kuleta mabadiliko chanya kwa wananchi.

Kati ya miradi hiyo, Mwenge wa Uhuru umeweka jiwe la msingi katika mradi mkubwa wa ujenzi wa maegesho ya magari makubwa katika eneo la Lilambo, mradi uliotengewa zaidi ya shilingi bilioni moja. Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea, Wakili Bashiri Muhoja, amesema hadi sasa zaidi ya shilingi milioni 223 zimetumika, na kwamba mradi huo ni kichocheo muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa eneo hilo.

Katika hatua nyingine ya kuboresha huduma kwa jamii, Mwenge wa Uhuru umefungua duka la dawa katika hospitali ya Mjimwema. Mradi huo unatarajiwa kugharimu zaidi ya shilingi milioni 68, fedha zilizotokana na

mapato ya ndani, na utasaidia kupunguza usumbufu kwa wagonjwa kupata dawa muhimu kutoka MSD.

Aidha, Mwenge wa Uhuru umetembelea mradi wa utunzaji wa kisima cha asili kilichopo Kata ya Matogoro, kilichoboreshwa kwa zaidi ya shilingi milioni 23.9 na sasa kinahudumia kaya zaidi ya 500 kwa kutoa maji bure. Mzee Mohamed Said, mzaliwa wa mwaka 1936, alitoa eneo hilo bure kuunga mkono juhudi za serikali katika kutoa huduma ya maji safi na salama.

Katika kusukuma mbele ajira na maendeleo kwa vijana, Mwenge wa Uhuru pia umetembelea kikundi cha Super Group cha Kata ya Ruvuma kilichonufaika na mkopo wa shilingi milioni 15 kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri. Kikundi hicho ni mfano wa mafanikio ya mikopo isiyo na riba kwa vijana.

Kwa upande wa nishati mbadala, Mwenge wa Uhuru umekagua mradi wa matumizi ya gesi katika shule ya Good Shepherd Montessori. Mkuu wa shule hiyo, Joshua Sonsoge, amesema matumizi ya gesi yanapunguza gharama za kuni kutoka milioni 4 hadi milioni 3 kwa mwaka, hatua muhimu katika kulinda mazingira na kupunguza matumizi ya rasilimali za misitu.

Katika kuhakikisha watendaji wanakuwa na vifaa vya kazi, Mwenge wa Uhuru umegawa pikipiki 17 na vishikwambi 16 kwa watendaji wa Kata, kwa gharama ya zaidi ya shilingi milioni 76, hatua inayolenga kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Akizungumza wakati wa mbio hizo, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2025, Ismali Ali Ussi, amepongeza uongozi wa Manispaa ya Songea kwa usimamizi madhubuti wa miradi ya maendeleo. “Katika Manispaa ya Songea tumeona miradi iliyopangiliwa vizuri, utekelezaji wa viwango na ushirikishwaji wa wananchi. Hii ni mfano bora,” alisema.

Amehimiza wananchi kuitunza miundombinu hiyo na kujitokeza kwa wingi katika uchaguzi mkuu mwezi Oktoba kwa amani na utulivu. Aidha, amesisitiza kuwa Mwenge wa Uhuru ni alama ya uzalendo na mshikamano wa kitaifa chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

## MWENGE WA UHURU WAANGAZA NAMTUMBO



Mwenge wa Uhuru ukiwa katika mbio zake mkoani Ruvuma, umeendelea kuangaza matumaini kwa wananchi kwa kupitia, kuzindua, na kuweka mawe ya msingi katika miradi ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 1.5 katika Wilaya ya Namtumbo pekee.

Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2025, **Ismail Ali Ussi**, amesema ameridhishwa na utekelezaji wa miradi mbalimbali katika wilaya hiyo, hususan miradi ya maji na elimu ambayo imeelezwa kuwa na ubora wa hali ya juu unaokidhi viwango vya kitaifa.

### Mradi wa maji wa bilioni 1.1 kuwaondolea wananchi kero ya maji

Katika hatua kubwa ya mapinduzi ya huduma ya maji safi na salama, Mwenge wa Uhuru umeweka **jiwe la msingi katika mradi wa maji wa Msisima** unaogharimu zaidi ya **shilingi bilioni 1.1**, ambao utahudumia wakazi **4,081** wa vijiji vya **Msisima na Mnalawi**.

**Mhandisi David Mkondya**, Meneja wa RUWASA Wilaya ya Namtumbo, amesema utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia **60**, na unatarajiwa kuondoa kabisa tatizo la upatikanaji wa maji safi katika vijiji hivyo.

**Madarasa mapya kupunguza msongamano**

Mwenge wa Uhuru pia umefungua rasmi **mradi wa ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na matundu sita ya vyoo** katika Shule ya Msingi Mtakanini, unaotekelezwa kupitia **programu ya BOOST** kwa gharama ya **shilingi milioni 107**.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Namtumbo, **Philemon Magesa**, amesema ujenzi huo unakwenda kupunguza kwa kiasi kikubwa **msongamano wa wanafunzi darasani**, hali inayoboresha mazingira ya ujifunzaji.

**Kituo cha mafuta na vifaa vya afya navyo vafaidika**

Katika kuimarisha huduma za kijamii na kiuchumi, Mwenge wa Uhuru umeweka jiwe la msingi kwenye **kituo cha mafuta cha Anchr Oil Mtwara Pachani** kilichopo Kata ya Luegu, kilichogharimu **takribani shilingi milioni 160** hadi sasa.

Aidha, Mwenge umekagua vifaa vya kisasa vya meno vikiwemo **dental chair** na **dental X-ray machine** vilivyonunuliwa kwa **shilingi milioni 18.94** kwa ajili ya **Kituo cha Afya Lusewa**, fedha zilizotokana na **mapato ya ndani** ya Halmashauri.

Mkurugenzi Magesa amesema vifaa hivyo ni hatua muhimu katika kuimarisha huduma za afya ya kinywa na meno kwa wakazi wa eneo hilo.

**Nishati safi yapelekwa kwa wananchi**

Katika jitihada za kuhamasisha matumizi ya nishati safi, Mwenge wa Uhuru umetoa **mitungi 20 ya gesi safi** yenye thamani ya **shilingi milioni moja** kwa wananchi wa Namtumbo. Magesa amesema Halmashauri inaendelea kutoa elimu kuhusu nishati safi ili kulinda afya na mazingira.

**Kiongozi wa Mwenge atoa pongezi kwa Serikali ya Wilaya**

Akihitimisha ziara hiyo, **Ismail Ussi** ameipongeza Serikali ya Wilaya ya Namtumbo kwa **kusimamia vizuri miradi ya kimkakati**, hasa miradi ya maji na elimu, akieleza kuwa ni hatua madhubuti za kumuunga mkono Rais **Dkt. Samia Suluhu Hassan**, ambaye amewezesha fedha nyingi kwa ajili ya miradi hiyo.

# MWENGE WA UHURU WARIDHIA MIRADI YOTE TUNDURU




Mwenge wa uhuru umekamilisha ziara yake mkoani Ruvuma kwa kuangazia miradi ya wilaya ya Tunduru ambapo umeweza kuweka jiwe la msingi katika mradi mkubwa wa maji safi na salama wa Masuguru unaogharimu Zaidi ya shilingi bilioni 2.4.

Mwenge wa Uhuru mwaka 2025 umezindua , kukagua, kutembelea na kuweka mawe ya msingi katika miradi 11 yenye thamani ya shilingi Bilioni 3.2 wilayani Tunduru

Meneja wa RUWASA Wilaya ya Tunduru Mhandisi Maua Mgallah amesema mradi huo uliofikia asilimia 85 ya utekelezaji unakwenda kuwanufaisha wananchi wapatao 16,124 na kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika wilaya hiyo kutoka asilimia 81.86 hadi kufikia asilimia 86.65.

Mwenge wa uhuru ukiwa wilayani Tunduru pia umeweka jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa jengo la kusubiria ndugu wa wagonjwa katika

hospitali ya wilaya ya Tunduru ambapo serikali imetenga Zaidi ya shilingi milioni 97 kutoka mapato ya ndani kutekeleza mradi huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru Chiza Marando amesema hadi sasa mradi umefikia asilimia 80 ya utekelezaji na kwamba mradi huo utawawezesha ndugu wa wagonjwa kutoa huduma mbalimbali kwa wagonjwa na kupunguza msongamano wa ndugu wa wagonjwa katika maeneo ya kutolea huduma hasa wodini.

Mwenge wa Uhuru ukiwa wilayani Tunduru pia umetembelea shamba la miti katika kijiji cha Chiwana lenye ukubwa wa hekari 8.23 ambalo limepandwa miti hekari 2,3 aina ya mitiki ambalo lina miti 1,551.

Mwenyekiti wa kijiji cha Chiwana Mohamed Chiulika amesema shamba darasa dogo hilo lilianzishwa mwaka 2021 kupitia mradi wa TASAF lengo likiwa ni kutunza mazingira kupitia upandaji miti.

Amezitaja baadhi ya faida ambazo zimepatikana hadi sasa kutokana na mradi huo ni pamoja na watu 50 kupata elimu ya upandaji miti na utunzaji wa mazingira,miti itakapokomaa kijiji kitaongeza mapato kupitia mbao na matumizi mbalimbali yanayotokana na miti hiyo yenye soko kubwa kimataifa.

Mwenge wa uhuru ukiwa wilayani Tunduru pia umetembelea mradi wa nishati safi ya kupikia katika shule ya sekondari Tunduru ambao unagharimu Zaidi ya shilingi milioni 24.

Katika sekondari ya Tunduru mwenge wa uhuru pia umepitia mradi wa ujenzi wa mabweni mawili na matundu sita ya vyoo.

Mwenge wa Uhuru ukiwa wilayani Tunduru pia umezindua mradi wa ujenzi w barabara ya nguzo sita-Muungano hadi Camp David yenye urefu wa kilometa 0.5 kwa kiwango cha lami unaotekelezwa na TARURA.

Meneja wa TARURA wilaya ya Tunduru Mhandisi Silnavus Ngonyani amesema mradi huo umegharimu Zaidi ya shilingi milioni 234.

Mwenge wa uhuru pia umepitia mradi wa ugawaji vyandarua kwa akinamama wajawazito na watoto wa miezi tisa ambapo mradi huo umegharimu Zaidi ya shilingi milioni 59 fedha ambazo zimetolewa na wahisani wa Global Fund.

Mwenge wa uhuru umekagua shughuli za lishe katika Halmashauri hiyo mradi ambao umegharimu shilingi 605,000.

Hata hivyo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo Chiza Marando amelitaja lengo la kupunguza na kuzuia tatizo la udumavu katika kipindi cha siku 1000 za mwanzo wa maisha ya mtoto ambapo Halmashauri hiyo imetenga shilingi milioni 70 katika kutekeleza afua za lishe.

Akizungumza kwa nyakati tofauti baada ya kupitia miradi hiyo kiongozi wa mbio za mwenge wa uhuru kitaifa 2025 Ndugu Ismali Ali Ussi amewapongeza viongozi wa Halmashauri hiyo kwa kusimamia ipasavyo miradi hiyo ambayo imetekelezwa katika ubora unaolingana na thamani ya fedha.

Ussi amewakumbusha wananchi wote waliojiandikisha kujitokeza kwa wingi kupiga kura Oktoba mwaka huu kwenye uchaguzi mkuu wa Rais,wabunge na madiwani.

## MAKABIDHIANO YA MWENGE WA UHURU KATI YA MKOA WA RUVUMA NA MTWARA



Mwenge wa Uhuru 2025 mkoani Ruvuma, umepitia na kuridhia jumla ya miradi 76 ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 95.

Taarifa hiyo imetolewa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Bi. Mary Gasper Makondo, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed, wakati wa hafla ya makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru kati ya Mkoa wa Ruvuma na Mtwara iliyofanyika katika viwanja vya Shule ya Msingi Lumesule, wilayani Nanyumbu mkoani Mtwara.

Mwenge wa Uhuru uliingia mkoani Ruvuma Mei 9 na kumaliza mbio zake Mei 16, ukipitia Halmashauri zote nane za mkoa huo kwa umbali wa kilomita 1,378.9.

Katika kipindi hicho, miradi yote 76 iliyotembelewa ilifanyiwa ukaguzi na hatimaye kupitishwa na timu ya wakimbiza mwenge kitaifa, ikiwa ni ishara ya mafanikio makubwa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayogusa maisha ya wananchi moja kwa moja.

Kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Katibu Tawala wa Mkoa huo, alikiri rasmi kupokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Bi. Mary Makondo na kuupongeza Mkoa wa Ruvuma kwa maandalizi mazuri na utekelezaji bora wa miradi.

Akihutubia hadhara hiyo, Bi. Makondo alieleza kuwa wananchi wa Ruvuma wamefaidika mno na mbio za mwenge wa Uhuru ambazo zimewaamsha katika kushiriki kikamilifu kwenye masuala ya maendeleo na kuwaasa kujitokeza kwa wingi katika uchaguzi mkuu 2025, sambamba na kauli mbiu ya mwaka huu isemayo *"Jitokeze Kushiriki Uchaguzi Mkuu 2025 kwa Amani na Utulivu."*

Aidha, Bi. Makondo alitumia fursa hiyo kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mchango wake mkubwa katika kuleta maendeleo mkoani Ruvuma kupitia fedha za utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati.

Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa barabara ya Mbinga–Mbamba Bay, upanuzi wa uwanja wa ndege wa Songea, ujenzi wa bandari ya Ndumbi (Nyasa), pamoja na upanuzi unaoendelea wa bandari ya Mbamba Bay.



Mbunge wa Peramiho ambaye pia ni Waziri wa Afya Mheshimiwa Jenista Mhagama alivyowaongoza wananchi wa jimbo lake kwenye mapokezi ya mwenge wa Uhuru 2025 eneo la mji mdogo wa Peramiho.



Miongoni mwa wananchi waliojitokeza kumsikiliza Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru 2025 Ndugu Ismail Ali Ussi mjini Tunduru.



Mwenge wa uhuru 2025 umezindua mradi wa ujenzi wa miundombinu ya vyumba vinne vya madarasa na matundu sita ya vyoo kupitia BOOST mradi huo umetekelezwa katika shule ya msingi Mtakanini wilayani Namtumbo mradi ambao umegharimu zaidi ya shilingi milioni 107



Mwenge wa uhuru umeridhia kuweka jiwe la Msingi katika mradi wa maji Mbanga katika Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma unaogharimu zaidi ya shilingi milioni 962.
Mradi huo unatarajia kunufaisha wananchi 4,490 ambao watapata maji safi na salama



Mwenge wa uhuru 2025 umeridhia kufungua mradi wa maji Mkwaya katika wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma ambao umegharimu zaidi ya shilingi milioni 375 na unawanufaisha watu 1,853 waliopo katika kijiji cha Mkwaya ambapo hadi Sasa kaya 13 zimeunganishwa na huduma ya maji majumbani





Mwenge wa uhuru 2025 umefungua mradi wa duka la dawa katika hospitali ya Mjimwema Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.
Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea Wakili Bashir Muhoja amesema hadi sasa mradi umegharimu zaidi ya shilingi milioni 68 ambazo zimetokana na mapato ya ndani



Mwenge wa Uhuru umeridhia kuweka jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa maegesho ya magari makubwa katika Kata ya Lilambo mjini Songea unaogharimu zaidi ya shilingi bilioni moja fedha zinazotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri hiyo ambapo hadi sasa mradi umetumia zaidi ya shilingi milioni 223



Mwenge wa Uhuru 2025 umeweka jiwe la msingi katika ujenzi wa shule mpya ya sekondari ya Jumbe IDD iliyopo Mtaa wa Namanditi, Kata ya Ruhuwiko, Manispaa ya Songea. mradi huo umegharimu zaidi ya shilingi milioni 658



**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA**
**Kupitia Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma**


S.L.P 74 SONGEA

57180 RUVUMA

SIMU Nambari. 025-2602256/2602238

FAX Na. 2602144

E -MAIL:ras.ruvuma@tamisemi.go.tz

TOVUTI: www.ruvuma.go.tz

INSTAGRAM: rs ruvuma

FACEBOOK: rs ruvuma

YOUTUBE: rs ruvuma